MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Nadharia ya Fasihi Mazingira: Mawanda na Matapo yake Katika Fasihi ya Kiswahili

Nixion Sangili*

*Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu cha Marafiki cha Kaimosi, Kenya.*

## IKISIRI

Tangu kuasisiwa kwa nadharia hii ya fasihi mazingira mwaka wa 1996 na Cheryl Glotfelty, watafiti na wahakiki wengi wa fasihi mazingira wamekuwa na tashwishi ya kuitumia katika uchanganuzi na uhakiki wa kazi zao. Hii ni kwa sababu nadharia hii imeonekana kuwa pana mno, na inayokosa mawanda maalumu na bayana. Baadhi ya wahakiki wamedai kwamba nadharia hii si ya kifasihi kwa sababu inaonekana kulazimishiwa katika fasihi. Hata hivyo, baadhi ya wataalamu waliowahi kutumia nadharia hii kama vile Glotfelty na Fromm kwa ustadi mkubwa wanaikolezea sifa kwa madai kwamba licha ya upana wake, kila mhakiki na mtumiaji wa nadharia hii ndiye wa kuamua jinsi atakavyoitumia katika utafiti wake. Kazi hii kwa hivyo, inachochewa na mjadala huu wa kuunga na kupinga matumizi ya nadharia hii katika fasihi, kwa lengo la kuonyesha mawanda yake halisi na kutoa maelekezo ya matumizi. Katika kutekeleza hili, kazi hii itatalii machapisho ya wataalumu mbalimbali waliowahi kuchangia mawanda na matumizi ya nadharia ya fasihi mazingira tangu kuasisiwa kwake mwaka wa 1978 hadi 2022. Aidha, utafiti utajaribu kuonyesha mawanda ya nadharia hii katika fasihi ya Kiswahili, kwa kurejelea machapisho yaliyowahi kuwasilishwa au kuchapishwa kuhusu fasihi ya Kiswahili. Aodha, mchango wake mkubwa umo katika kukusanya matapo au mirengo yake mbalimbali katika chapisho la Kiswahili linaloweza kutumiwa kama marejeleo.

## KUHUSU MAKALA

*Maneno Muhimu:*
Fasihi Mazingira,
Nadharia,
Uhakiki.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 1 Februari 2026
Tarehe ya Kurekebishwa: 21 Marchi 2026
Tarehe ya Kukubalika: 24 Machi 2026
Mtandaoni: 8 Machi 2025

## 1. Utangulizi

Dhana ya fasihi mazingira imekuwepo tangu mwaka wa 1978 wakati kitabu cha William Rueckert "*Literature and Ecology: An Experiment in Eco-criticism*" kilipozinduliwa. Rueckert (1978) alikuwa na lengo la kuonyesha jinsi ekolojia na dhana za kiekolojia au kimazingira zingeweza kutumika katika uhakiki wa fasihi (Emmanuel & Ngozi, 2015). Inakisiwa kwamba, hata kabla ya mwaka huo wa 1978, kulikuwepo na watunzi waliokuwa wametunga fasihi iliyokuwa inaegemea mazingira asilia japo hawakuwa na wazo kuhusu fasihi mazingira. Maudhui na ususi wa mitindo ya masimulizi, ujenzi wa wahusika na vitushi ni mambo yaliyokuwa yanajitokeza katika kazi za hawa watunzi (Buell, 2005). Wingu hili jipya katika fasihi lilizidi kukua, na, Cherryl Glotfelty & Fromm (1996), walianzisha nadharia rasmi ambayo ingeongoza ndaro za utunzi na uhakiki wa kazi zilizoanza kuainishwa kama kazi za fasihi kimazingira. Mfumo huu wa uwazaji waliuita Nadharia ya fasihi mazingira.

Tangu kuasisiwa kwake Marekani, fasihi hii ilianza kusambaa ulimwenguni kote kuanzia Uingereza, Italia, Uhispania na Ulaya nzima (Hartmann, 2007; Buell, Heise & Thornber, 2011): bara la Asia na hatimaye, bara la Afrika (Egya, 2020). Kutunukiwa Tuzo la Nobel kwa marehemu Wangari Maathai, kulichapua mkondo huu barani Afrika, hususan nchini Kenya (Mwangi, 2004)

## 2. Nadharia ya Fasihi Mazingira

Nadharia ya fasihi mazingira inalenga kuonyesha uhusiano uliopo kati ya fasihi na mazingira asilia. Inalenga kusaili masuala yafuatayo:

i. Je, mazingira asilia yanaathiriwa kwa jinsi gani na wanadamu (wahusika) katika matini ya kifasihi?
ii. Je, wanadamu (wahusika) wanaathiriwa kwa jinsi gani na mazingira asilia katika matini ya kifasihi?
iii. Je, wanadamu (wahusika) wanawajibikia vipi mazingira asilia katika fasihi?
iv. Mambo/maudhui gani yanaibuka katika mwingiliano wa binadamu (wahusika) na mazingira asilia katika fasihi?
v. Je, matini ya fasihi inachochea msomaji kuangalia mazingira asilia au anajikuta anajifunga tu kwa wahusika wa kibinadamu?

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: nsangili@kafu.ac.ke
Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Sangili N. (2026). Nadharia ya Fasihi Mazingira: Mawanda na Matapo yake Katika Fasihi ya Kiswahili. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(1), 9 – 14. https://doi.org/10.61889/je3p5b16.

© 2026 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

vi. Je, matini ya kifasihi inazua ufahamu wa mazingira asilia, na msomaji anajinasibisha nayo kwa namna gani?
vii. Fasihi huchochea vipi mawazo ya kimazingira na mabadiliko ya tabianchi inaposomwa na hadhira?

Hoja hizi kuu, ambazo pia ni kama mihimili jumla ya nadharia hii, zinajaribu kuonyesha uhusiano uliopo kati ya fasihi na utunzaji wa mazingira asilia. Anavyosema Kwaku (2005), fasihi inatumika kisanii kuokoa mazingira asilia. Kuwepo kwa vipopo vya fasihi simulizi vinavyotokana na mazingira asilia, kuwepo kwa mila zinazoandamana na mazingira, pamoja na matukio mengine ya kimazingira yanayofungamana na fasihi, pia ni ishara tosha kwamba mazingira asilia yanaathiri fasihi; na fasihi hii inastahili pia kuathiri mazingira, japo kichanya. Kwaku (2005) anazidi kusema kwamba mazingira asilia hayaathiriwi tu na nguvu asilia kama vile mvua, upepo na jua bali pia na imani na tamaduni za wanadamu. Aidha, kwa kiasi kikubwa, fasihi ni fumbato la tamaduni hizi. Kulingana na wanasayansi mazingira, matendo ya binadamu - ambayo yanatokana na falsafa ya utamaduni wake, ndio vichapuzi vikubwa vya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Utamaduni wa kujitakia makubwa, ujasiriamali usiopoozeka, upanuzi wa miji, usayansishaji wa kilimo na teknolojia za maji, ardhi na anga, zimesababisha ongezeko la mvuguto; hivyo basi, kuchangia pakubwa kupanda kwa viwango vya joto ulimwengu mzima.

## 3. Mawanda ya Matumizi ya nadharia ya fasihi mazingira

Nadharia ya fasihi mazingira kama nadharia ya uhakiki wa fasihi, ni uwanja ambao ungali unabadilika na kupanuka. Kwa mujibu wa Emmanuel & Ngozi (2015), kungali na mapendekezo, madhanio na matapo yanayozidi kuongezewa nadharia hii ya kipekee katika fasihi. Kwa mfano, katika fasihi ya Kimagharibi, tapo jipya la fasihi tiba mazingira au bibiliotherapia limeanzishwa na linajengewa uhakiki. Wataalamu mbalimbali wanashikilia kuwa uwanja huu unashughulikia mawanda mapana. Baadhi ya mawanda haya ni kama vile: tanzu mbalimbali za fasihi (Sangili & Sabula, 2019), filamu/sinema na uigizaji (Rayson, 2014), Masomo ya Runinga (Ward & Vuuren, 2014), Futuhi ya vibonzo (Pike, 2014), utamaduni wa jamii (Nirmal, 2014) na mitandao/majukwaa ya kijamii, hasa blogu (Deborah, 2014). Mawanda haya yote kwa kiasi kikubwa yanahusiana, kwa sababu yanatumia lugha kibunifu kuweza kufikia hadhira lengwa.

Katika fasihi, nadharia hii hulenga kuchanganua maudhui, mazingira/mandhari, wahusika na vihusika, ujenzi wa falsafa ya utunzaji au uharibifu wa mazingira, lugha na itikadi ya utunzaji/uharibifu wa mazingira miongoni mwa masuala mengine. Kwa mfano, katika lugha, mhakiki wa uwanja huu huangalia jinsi lugha imeumbwa kutokana na mazingira asilia ya eneo fulani. Mhakiki huangalia pia namna ambavyo watunzi wamejenga jazanda kutokana na mazingira ambayo yanawazunguka. Hii hudhihirisha uhusiano na umuhimu wa mazingira asilia katika mchakato wa utunzi wa kazi ya kifasihi.

Katika mawanda ya kinadharia, fasihi mazingira imejichukulia mawanda ambayo ni ya kiwakati: kwa maana kwamba kuna mawanda mapya ya kinadharia yanayozidi kuibuka kila baada ya kipindi fulani. Nadharia hii ilipoanzishwa nao Glotfelty & Fromm (1996) na Buell (1996), ilikuwa na matapo finyu, yakiwemo: fasihi mazingira Kimarekani na fasihi mazingira kijiografia. Baadaye, ilipoanza kusambaa katika fasihi za kilimwengu, matapo mapya yaliongezwa. Kwa mfano, fasihi mazingira Kiulaya (Garrard, 2004), fasihi mazingira Kiasia; fasihi mazingira kimiji; fasihi mazingira Kiafrika, fasihi mazingira kiharakati; fasihi mazingira kibepari; fasihi mazingira kifeministi na fasihi mazingira kisoshalisti miongoni mwa mengine mawanda haya yamekuwa yakitumiwa na wahakiki mbalimbali kutegemea aina za kazi, eneo la kijiografia ambamo kazi fulani ya kifasihi imezaliwa ndani, mifumo ya uzalishaji mali wa jamii maalumu na miegemeo ya kijinsia. Tutaangalia kila mojawapo ya mawanda haya na kuonyesha mihimili yake kwa muhtasari pamoja na waasisi wake

### 3.1. Tapo la Fasihi mazingira ya Kimarekani

Fasihi ya Kimarekani ilianza kukumbatia nadharia hii kama mwitiko mpya uliofungamana na kazi mpya za kifasihi zilizokuwa zinaibuka, japo zilikuwa zimetungwa kabla ya 1996 (Glotfelty & Fromm, 1996; Buell, 2005; Buell, Heise & Thornber, 2011 na Indriyanto, 2020). Baadhi ya kazi zilizokuwa zimetungwa miaka ya awali ni kama vile, *The New English Canaan (1637)* na *Nature (1836),* zao Thomas Morton na Waldo Emerson, mtawalia. Mkondo huu ulikuwa mpya katika Taaluma za Usomi wa Kimarekani, na ulishikilia kwamba sanaa za ubunaji zinazotumia maneno zinaweza kuchangia pakubwa katika uelewaji wa uharibifu wa mazingira. Aidha, walikuwa na msimamo kwamba mazingira asilia ni sehemu ya fasihi ya Marekani na, kwa hivyo, haiwezi kuchukuliwa kama kijipengele tu cha uhakiki (Indriyanto, 2020).

Uwazaji huu ulitokana na historia ya ukoloni Marekani kuanzia karne ya 17 hadi karne ya 20 ubepari uliposimika kwa kina na kasi. Watalaam hawa ((Glotfelty & Fromm, 1996; Buell, 2005; Buell, Heise & Thornber, 2011) walihisi kwamba utamaduni wa Marekani umeathiri na kuathiriwa na mazingira asilia. Matatizo ya kimazingira japo yalikuwa yanasomwa katika sayansi asilia, yalikuwa yanaathiri watunzi na Wamarekani wote. Hivyo, waanzilishi wake wakazua suala la namna ambavyo Fasihi ya Marekani inaweza kuchangia katika kuhamasisha na kuzua mwitiko chanya miongoni mwa wanafasihi kuhusu utunzaji wa mazingira, uamshaji wa ari na ung'amuzi kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

Baadhi ya vipengele ambavyo vinahakikiwa kupitia mkabala huu wa Kimarekani ni: wahusika/vihusika; mandhari; lugha ya kifasihi/kimazingira; ubepari unavyoathiri mazingira; umijiishaji wa Marekani; kuongezeka kwa matumizi ya kemikali katika ukulima, na masuala mengine mbalimbali. Ni kutokana na mawazo haya ambapo Chama cha Fasihi mazingira Marekani yaani, *Interdisciplinary Studies in Literature and Environment*. (ISLE) kilizinduliwa na baadaye

wakaanzisha jarida la *Interdisciplinary Studies in Literature and Environment* (ISLE) mwaka wa 1993. Jarida hili lilishughulikia masuala ya mazingira asilia katika fasihi ya Marekani.

### 3.2. Tapo Fasihi mazingira ya Kiulaya

Mkabala huu ulianzishwa kama mwitiko wa mwingiliano-diskosi kati ya wanafasihi wa Kimarekani na wa Kiulaya, hasa Uingereza ambapo ndio mwanzo wa mkondo wa Kiulaya. Katika kuanza kwake Ulaya, mkabala huu ulishabihi ule wa Kimarekani. Hata hivyo, wahakiki wa Ulaya walianza kutofautiana na wenzao wa Kimarekani (Goodboy, 2011). Kwa mfano, mkabala wa Kiulaya ulianza kutilia mkazo lugha, mfumo wa kimasimulizi na umbo la kazi ya kifasihi. Masuala haya hayakuwa yanapewa kipaumbele katika mkabala wa Kimarekani. Aidha, wanaulaya walitilia mkazo zaidi uhusiano kati ya mazingira asilia, utamaduni, fasihi na historia ya kila taifa la Ulaya. Waliamini kwamba tofauti na Marekani, kila taifa la Ulaya lilikuwa na historia ya kipekee kuhusu ukoloni, vita, ukuaji wa viwanda na ung'amuzi kimazingira. Goodboy (2011) anaeleza kwamba, fasihi mazingira ya Kimarekani ilikuwa inapendelea sana suala la nyika katika fasihi; ~~na~~ lakini upande wa Wanaulaya, kipengele hiki hakikuwa katika jumla ya mawazo ya fasihi ya Ulaya. Hii ndiyo sababu wanapochunguza fasihi mazingira ya Ulaya, Goodboy, Junquera & Uppermann (2020) wanatambua upekee wa Ufaransa, Italia, nchi za Skandinavia, Ujerumani, Uhispania na nchi zingine za Ulaya. Kwa mfano, walitambua kwamba wanafasihi wa Kifaransa wanagemea ushairi (masimulizi, semiotiki, umitindo na isimu); Waitalia wanazingatia maadili na ujumisia unaofungamana na uharibifu wa mazingira. Katika taifa la Ireland, wahakiki walianza kuchunguza utambulisho wa kitaifa uliomo katika kazi za kimazingira; ila sasa wameanza kusoma upya kazi hizo na kuziegemeza kwenye falsafa ya mwamko wa kimazingira (Goodboy, Junquera & Uppermann, 2020).

Fasihi mazingira ya Ulaya inatazama mazingira kama jukumu la kitamaduni kuliko la mtu binafsi. Kuwepo kwa lugha nyingi Ulaya, uanuwai-jamii na uanuwai-tamaduni unaosaidia kuelewa mwingiliano wa binadamu na mazingira asilia ni muhimu sana wanapohakiki upekee uliomo kwenye mkabala huu. Aidha, tofauti na mkabala wa Kimarekani uliokuwa na msingi katika Taaluma za Usomi wa Kimarekani, Wanaulaya waliegemeza mkabala wao kwa ulimbwende wa Kiulaya. Walitaka kuonyesha jinsi mazingira na utamaduni yanahusiana na sanaa katika kuvyaza ufikiriaji kuhusu mazingira asilia. Ni kutokana na haya yote basi Wanaulaya wakaamua kuchukua baadhi ya vipengele vya nadharia za Umuundo, Fenomenolojia, Umaksi, Ufeministi, Upokezi, na Bayosemiotiki, kwa minajili ya kuboresha mkabala wa Fasihi Mazingira Kiulaya (Goodboy, Junquera & Uppermann, 2020).

### 3.3. Tapo la Fasihi mazingira ya Kiafrika

Huu ni mkabala unaolenga kuchunguza kazi mbalimbali za kifasihi zilizowahi kutungwa kwa mtazamo wa kimazingira barani Afrika. Kulingana na Egya (2020), bara la Afrika, hasa mataifa yaliyo kusini mwa Sahara, yana upekee wake unaostahili kuzingatiwa na wenyeji badala ya wageni, ambao wanapotosha kwenye taarifa zao kuhusu eneo hili. Anadai kwamba tafiti za kimagharibi kuhusu fasihi mazingira katika eneo hili zimechora taswira ya bara ambalo kimazingira, lina maskini wengi wanaoharibu mazingira. Chambilecho Egya (2020) upekee uliomo katika eneo hili unaostahili kuchunguzwa ni: athari za ukoloni kwa mazingira na jinsi watunzi wa fasihi wanachimuza suala hili; upekee uliomo katika misitu, vyanzi vya maji na utajiri wa mazingira asilia unavyojitokeza au kuchangia vipopo vya kifasihi; utamaduni-anuwai wa kila jamii eneo hili la kusini mwa Sahara. Mwisho, kuwepo kwa jamii nyingi barani Afrika na jinsi jamii hizi zinausiana, moja kwa nyingine; na ~~pia~~ jinsi zinavyohusiana na mazingira asilia yanayowazunguka.

Mawazo haya yanatiliwa pondo na utafiti wa Kwaku (2005) aliyetambua kwamba fasihi mazingira ya Kiafrika, na hususan Ghana, inaonyesha ukwasi mkubwa wa kiuhusiano baina ya wanajamii na mazingira asilia kama vile miti, mito, ndege na viumbe wengine. Egya (2020) anasisitiza kwamba fasihi ya kimazingira, mkabala wa Kiafrika, unastahili kuangalia jinsi ambavyo taasisi za ndani na nje ya bara hili zimehusika katika kutunza na kuharibu mazingira. Aidha, wahakiki waangalie jinsi tamaduni za Kiafrika zinavyaza ufikiriaji wa kipekee wa kifasihi unaofungamana na mazingira asilia. Kwa mfano, Sangili (2014) anaonyesha wazi jinsi methali, tamathali, nahau na nyimbo za fasihi simulizi ya Wamaragooli wa Kenya zinahusiana pakubwa na utamaduni wa Mwafrika katika kuingiliana na mazingira yake asilia. Kwa hivyo, katika kuchunguza fasihi kwa kutumia mkabala huu, mhakiki aangalie maudhui ya Kiafrika yanavyojitokeza, lugha inavyoumbwa kutokana na mazingira asilia; pamoja na ujenzi wa wahusika/vihusika kutokana na nguvu na mahusiano ya kimazingira miongoni mwa masuala mengine.

### 3.4. Tapo la Fasihi mazingira ya Kifeministi

Chambilecho Sabula & Sangili (2019), fasihi mazingira kifeministi pia huitwa fasihi mazingira kinisai. Huu ni mkabala uliochipuka kutokana na juhudi za wanaharakati wa ufeministi. Neno hili lilitumiwa kwanza na Francois d'Eaubonne mwaka 1974 ili kuonyesha mwingiliano wa ufeministi na mazingira. Mkabala huu ulipanuliwa kadiri ulivyozidi kukua duniani, na hadi sasa kuna mitazamo mbalimbali, kama vile: fasihi mazingira kinisai kwa mtazamo wa kimaksi, kiharakati, kidhanaishi, kisaikolojia-changanuzi, kijamii, na kiusasa-leo (Warren, 2000). Mitazamo hii yote inapania kuonyesha jinsi kazi ya kifasihi inavyochunguza na kuwasilisha masuala ya kimazingira asilia kwa kuegemea ufeministi (Shiva & Mies, 1993; Warren, 2000 ; Sabula & Sangili, 2019).

Wahakiki wa mtazamo huu huangalia mambo yafuatayo: usawiri wa mwanamke katika harakati za utetezi au uharibifu wa mazingira asilia; idadi ya wanawake wanaojihusisha na juhudi za uhifadhi mazingira katika jamii maalum; changamoto ambazo mwanamke mtetezi wa mazingira anapitia katika kutekeleza majukumu yake; mbinu za kumkomboa

mwanamke dhidi ya unyanyasaji wa kimazingira; falsafa na itikadi za kiutawala zinavyomkabili mwanamke anayetaka kujihusisha na harakati za kimazingira miongoni mwa masuala mengine. Kimsingi, Shiva & Mies (1993) wanadai kwamba matatizo ambayo mwanamke anapitia – yakiwemo unyanyasaji, ukandamizaji na kutusiwa, ni yayo hayo ambayo mazingira asilia yanapitia. Hivyo basi, kumkomboa mwanamke ni sawa na kukomboa mazingira asilia.

### 3.5. Tapo la Fasihi mazingira ya Kisoshalisti

Mkabala huu wa kinadharia ulianzishwa naye Murray Bookchin mwaka wa 1996, ambaye ni mwanamazingira na mwanaharakati wa kijamii (Singh, 2019). Mkabala huu unaangalia jinsi muundo wa kijamii unavyochangia uongozi na uharibifu wa mazingira. Kuwepo kwa ngazi mbalimbali za kiutawala kunaathiri jinsi wanajamii wanaingiliana na kuhusiana na mazingira asilia yanayowazunguka. Taasisi mbalimbali pia zinaathiri kichanya au kihasi, mazingira asilia. Wanaoshabikia mkabala huu wanadai kwamba kuna haja ya kufikiria na kuunda upya masuala ya utawala katika jamii ili ziweze kutilia maanani mazingira asilia. Badala ya kuwepo kwa kiongozi dikteta, pawepo na demokrasia ambapo jamii nzima inahusishwa kwenye maamuzi yaliyo bora. Aidha, katika mifumo ya uzalishaji mali, pawepo na ubia wa kuhodhi mali badala ya ubepari unaotenga baadhi na kuwafanya wengi kuwa maskini, hivyo basi kuchochea uharibifu wa mazingira. Hivyo, katika kuangalia kazi za fasihi, haya masuala yaweze kuchunguzwa kwa makini na kutoa suluhisho la kisoshalisti linalonawirisha na kulinda mazingira asilia.

### 3.6. Tapo la Fasihi mazingira ya Baada-Ukoloni

Huu ni mkabala wa kipekee katika nadharia hii pana ambayo inajumuisha nadharia mbili zilizo na mawazo tofauti: nadharia ya fasihi mazingira na ya baada-ukoloni. Kwa mujibu wa Huggan & Tiffin (2010), nadharia hizi mbili ziliungana kupinga uendelezwaji kibabe wa ubepari wa kijamii na kimazingira ambao ungali unaendelea hadi sasa. Wahakiki wanaotumia mkabala huu huchunguza jinsi wazo la kimagharibi la utunzaji wa mazingira katika mataifa yanayostawi hupuuza tamaduni za kale au kiasili za wenyeji pamoja na mazingira yao.

Fasihi mazingira ya baada-ukoloni huchunguza athari za ukoloni, za baada ya ukoloni na ubabe wa kiutandawazi wa mataifa yaliyostawi. Mkabala huu husisitiza kwamba mazingira asilia ni amana ya kijamii na hayafai kuharibiwa kiholelaholela kwa kuwa yamelindwa na sheria kwa manufaa ya jamii nzima (Gebrehiwot, 2020; Jonah, 2020). Jinsi wenyeji walivyopigania uhuru dhidi ya mkoloni katika sehemu mbalimbali za ulimwengu, mkabala huu unajaribu kusisitiza wazo la wenyeji kujiweka huru dhidi ya mawazo babe ya wakoloni wao kuhusu namna ya kutunza mazingira. Fauka ya hayo, wakoloni hawa wanazidi kuleta mifumo na teknolojia inayokandamiza mazingira yenyewe. Kila wanapoleta mifumo yao ya kimagharibi, mifumo ya wenyeji, hasa ile ya kitamaduni, inadidimizwa na kubezwa kuwa ni ya kale na haina manufaa kwa juhudi za kisasa za kisayansi katika utunzaji mazingira na upunguzaji wa athari kali za tabianchi. DeLoughrey (2014) anasema kuwa, lengo la mkabala huu ni kuumba upya ukale jinsi ulivyokuwa kabla ya kuja kwa mkoloni ili kumtanababhisha Mwafrika kuhusu mazingira yake, hivyo basi kumsababisha ayatunze pasipo kujilazimishia mifumo ya kikoloni.

### 3.7. Nadharia za fasihi mazingira: Maoni ya Kihakiki

Kuwepo kwa mambo mengi yaliyopakiziwa nadharia hii, kumeifanya ionekane pana mno kama wanavyodai baadhi ya wataalamu (Singh, 2019; Schliephake, 2015; Habeeb & Habeeb, 2012). Hali hii inasababisha uchangamano katika kuitumia nadharia hii katika uhakiki wa kazi ya fasihi. Hata hivyo, kwa wengine, nadharia hii~~,~~ haina utata wowote katika matumizi (Goodboy & wenzake, 2011; Emmanuel & Ngozi, 2015). Yamkini, kama tulivyoonyesha kwenye wasilisho hili, mhakiki ana nafasi ya kujichagulia mkabala anaotaka kuchukua katika kuhakiki kazi yake. Hivyo, hapafai kuwa na utata au uchangamano wowote kuhusiana na matumizi yake. Kwa mujibu wa Hawking (1998), ubora au udhaifu wa nadharia hutegemea mambo kadhaa. Kwanza, nadharia huwa bora iwapo inatimiza mambo yafuatayo: ina mtiririko wa mawazo na sehemu zake mbalimbali zinachangiana kujibu maswali mahsusi ya kinadharia; nadharia inatoa maelezo maanifu kwa maswali ibuka; inaweza kupembuliwa kisayansi; inasisimua ufikiriaji bunifu na utafiti mpya; inaeleza shani tunazozijua katika jamii; ina upeo unaoelezeka na inaweza kueleza mwingiliano wa masuala mbalimbali ya kijamii. Ni wazi kwamba nadharia hii imetekeleza hayo yote.

Adamczewski (2019) anapohakiki nadharia hii, anasema kwamba inadhihirisha mwingiliano-taaluma mkubwa kwa sababu inajaribu kueleza jinsi fasihi inahusiana na kuchangia utunzaji mazingira kwa kuangazia matatizo ya binadamu yanayotokana na uharibifu wa mazingira. Hivyo, hii inadhibitisha kile ambacho Hawking (1998) anaeleza kuhusu nadharia bora, kuwa ionyeshe uanuwai, itoe maelezo fanifu, inasisimua ufikiriaji bunifu na utafiti mpya. Mawazo haya pia yanashabikiwa na Oppermann (2016) anayedai kwamba katika kuhakiki nadharia ya fasihi mazingira, uzingatiaji wa mkabala wa kiusasaleo unaohusu mazingira ni muhimu. Mkabala huu unasisitiza wanafasihi mazingira na wahakiki kwa jumla wachunguze na kutafiti mifumo ya kisasaleo (kama vile utawala wa kiimla na mawazo ya kikoloni yanayosisitiza uwekezaji zaidi wa kiviwanda na kiteknolojia) inayokandamiza jamii katika masuala ya mazingira.

### 3.8. Matumizi ya nadharia ya Fasihi mazingira katika fasihi ya Kiswahili

Fasihi ya Kiswahili ni mojawapo ya fasihi zinazosambaa ulimwenguni kutokana na kuenea kwa Kiswahili. Hii ni kutokana na tafsiri nyingi za Kiswahili zilizofanyiwa kazi za kifasihi za lugha kuu mbalimbali duniani kama vile: Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kijerumani. Kwa mfano, Die Sklaverei der Gewürze (Kasri ya Mwinyi Fuad) na Die Kinder der Regenmacher (Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka). Hii ina maana kwamba upya wowote unaojitokeza katika fasihi hizi, sharti uakisiwe kwenye fasihi ya Kiswahili vilevile. Fasihi

mazingira kama uwanja wa uhakiki wa fasihi ya Kiswahili, umekuwa katika fasihi ya Kiswahili tangu mwaka wa 2011 ulipodahiliwa na utafiti wa Sangili uliowasilishwa katika kongamano la Chama cha Kiswahili Afrika Mashariki (CHAKAMA), mjini Nakuru nchini (Kenya). Baadaye, kazi za wasomi mbalimbali wa Kiswahili zikiwemo Ngala & Sangili (2014), Ngala (2014), (Sabula, 2014), Olali (2018), Sabula & Sangili (2019), Kobia & Njeru (2019), Wesonga, Ambuyo & Chimerah (2020), Bulaya & Mhango (2020), Njeru, Kobia & Musyimi (2022), miongoni mwa nyingine, ziliweka msingi thabiti na kuhakikisha kwamba uwanja huu umesambaa katika fasihi ya Kiswahili. Kazi ambazo zinajengwa sasa hivi zinatokana na msingi huu wa tafiti na machapisho mbalimbali. Hii ni ishara tosha kwamba fasihi ya Kiswahili, ina mizani sawa na fasihi za lugha kuu kama vile Kiingereza, Kihispania, Kiitaliano, Kijerumani na Kichina, zilizo na machapisho mengi kuhusu uwanja huu. Zaidi ya hayo, ni muhimu kufahamu kwamba, fasihi mazingira ya Kiswahili, inachangia mikondo mbalimbali ya fasihi mazingira.

Masuala ambayo yamechanganuliwa na watafiti hawa kwa kutumia nadharia hii (katika mikabala yake mbalimbali) ni kama vile: maudhui ya uharibifu wa mazingira; athari za uharibifu wa mazingira; ujenzi wa wahusika wanaotekeleza wajibu wa kimazingira (Sabula, 2014); mizozo ya kijamii inayotokana na mazingira (Kobia & Njeru, 2019); nafasi ya mwanamke katika kutetea mazingira (Sabula & Sangili, 2019) na jinsi fasihi ya watoto inavyofanikisha uwasilishi wa masuala ya kimazingira (Bulaya & Mhango, 2020). Kazi hizi zote zinaonyesha kwamba; kwanza, utunzi wa fasihi ya kimazingira umepiga hatua kubwa katika fasihi ya Kiswahili. Pili, wataalamu wa Kiswahili wamekumbatia mwelekeo mpya wa kinadharia katika fasihi. Tatu, kuna mwamko mpya wa watunzi na wahakiki wa Kiswahili kushiriki katika juhudi za utunzaji, urekebishaji na urudishaji mazingira katika hali yake ya awali.

## 4. Hitimisho

Fasihi inazidi kukua na kujitwalia mambo na majukumu mapya kila baada ya kizazi. Kuibuka, kukua na kusasishwa kwa uwanja na nadharia ya fasihi mazingira ni ishara tosha kwamba fasihi katika jamii inazidi kuwa na mchango mkubwa, sio tu kwa kukuza wahusika, lugha, mitindo au masuala ya kifasihi; bali pia katika kuhamasisha jamii kuhusu mambo yanayojiri na kubadilisha jamii na miundo yake yote. Fasihi mazingira kama ilivyoonyeshwa kwenye makala hii, ni nadharia moja yenye mikabala kadhaa ambayo kwa hakika, inaleta utajiri wa uhakiki na utathmini wa kazi yoyote ya kifasihi. Kutegemea matilaba yake, mhakiki anaweza kuteua mkabala wa Kimarekani, Kiulaya, Kiafrika, Kifeministi, Kisoshalisti au hata baada-ukoloni ili kuchanganua, kuchambua, kutathmini, kujadili au kuchunguza kazi yoyote ya kifasihi ikiwemo simulizi, andishi, ya mtandaoni, filamu, maigizo ya runinga/redio, na vibonzo miongoni mwa zingine.

## Marejeleo


Adamczewski, T. (2019). Weakness, Lameness and Veering. On the Practical Dimensions of Theories of Ecocriticsm. Uniwersytet Adama Mickiewicza

Buell, L. (1996). The Environmental Imagination: Thoreau, Nature Writing and the Formation of American Culture. London: Harvard University Press.

Buell, L. (2005). The Future of Environmental Criticism: Environmental Crisis and Literary Imagination. Oxford: Blackwell.

Buell, L., Heise, K. & Thornber, K. (2011). Literature and Environment. The Annual Review of Environment and Resource 2011.36:474- 440. USA: Harvard University Press.

Bulaya, J. & Mhango, M. (2020). Ujitokezaji wa Maudhui ya Utunzaji wa Mazingira katika Hadithi Teule za Watoto: Mifano kutoka Fasihi ya Kiswahili. Mulika Na. 38, Dar es Salaam.

DeLoughrey, E. (2014). Postcolonialism. In, The Oxford Handbook of Ecocriticism, G. Garrard (ed), Oxford: Oxford University Press pp. 321-340.

Deborah, S.S. (2014). Eating Out of Your Hands: Food Blogging as Transecological Phenomenon. In, Culture and Media: Ecocritical Explorations. Cambridge Scholars Publishing pp: 222-240

Egya, S.E. (2020). Out of Africa: Ecocriticism Beyond the Boundary of Environmental Justice. Ecozon, Vol.11 (2) pp 66-73. Alcala University.

Emmanuel, A. I. & Ngozi, B.M. (2015). Eurocentrism and The African Flora and Fauna: An Eco-Critical Discourse of Obinkaram Echewa's the Land's Lord. European Journal of English Language, Linguistics and Literature Vol. 2 No. 1, 2015, pp: 32-42

Garrard, G. (2004). Ecocriticism. London: Routledge.

Gebrehiwot, D. A. (2020). A Post-colonial Ecocritical Reading of Ecological Violence and Resistance in Selected Anglophone African Novels (2000-2010). PhD Thesis (unpublished). Addis Ababa University

Glotfelty, C. B., & H. Fromm. (1996). The Ecocriticism Reader: Landmarks in Literary Ecology. London: University of Georgia Press.

Goodboy, A. H., Junquera, C.F. & Oppermann, S. (2020). Introduction: 2020 Ecocriticism, in Europe and Beyond. ECOZON@ Vol. 2(2). https://doi.org/10.37536/ecozona.2020.11.2.4027.

Goodboy, A.H. (2011). Ecocritical theory: New European approaches. In, Ecocritical Theory: New European Approaches. In, Goodboy, A. Rigby, C.E. & Rigby, K. (eds) (2011). Virginia: University of Virginia Press. PP: 322-340.

Habeeb, G. & Habeeb, D. (2012). Eco-Critical Theory or E-Theory: Some Newer Perspectives. Proceedings of National Seminar on Postmodern Literary Theory and Literature, Nanded: Hyderabad. PP 12-14

Hartmann, S. (2007). The Rise of American Ecoliterature. Journal of American Studies in Scandinavia, Vol 55 (1) CBS: Copenhaggen. PP 31-58.

Hawking, S. (1998). Brief history of time. New York: Bantam Books.

Huggan, G. & Triffin, H. (2010). Postcolonial Ecocriticism: Literature, Animals, Environment. London: Routledge.

Indriyanto, K. (2020). American Studies and Ecocriticism: Post-National American Nature Writing. Journal of English Studies 23:101-116

Jonah, C.M. (2020). A Critical Analysis of Issues in Postcolonial-Ecocriticism.In, Ibadan Journal of Humanistic Studies Vol. 30: 37-51.

Kobia, J.M. & Njeru, M.K. (2019). Usawiri wa Mizozo ya Ardhi katika Riwaya ya Kiswahili: Mfano kutoka Riwaya ya Kufa Kuzikana. Koja la Taaluma za Insia. Ponera, A. & Badru, Z. (2019). Dar. Es Salaam: Karljamer Pubishers.PP: 355-376.

Kwaku, A. (2005). Ecocrticism and Environmental Knowledge of Asante Oral Traditional Poetry. M.A Thesis (unpublished), Witwatersrand University: Johannesburg

Mwangi, E. (2004). Nobel Prize: A Shot in the Arm for African Ecocritism. The Association for the Study of Literature and Environment. Nevada: ASLE.

Ngala, O. (2014). Uhakiki wa Suala la Uhifadhi wa Mazingira katika Tanzu Teule za Fasihi ya Kiswahili ya Milenia Mpya. Tasnifu za Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Maseno

Nirmal, P. (2014). The Dynamics of Using Open Source Media to Preserve Indigenous Cultures. Culture and Media: Ecocritical Explorations. Rayson, K.A., Deborah, S. S. & Sachindev, P.S. (eds) (2014). Cambridge: Cambridge Scholars Publishing. PP: 114-130.

Njeru, M., Kobia, J. & Musyimi, D. (2022). Usawiri wa Motifu za Kimazingira katika Tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya Majira ya Utasa (Arege, 2015). Katika, Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 5 (1), 151-160.

Olali, T. (2018). Ecology as Thematic Foci: The Identity of Swahili Poetry and Ecocriticism Experiment. Enviroment of African Literature. Washington D.C.: Marriot Wardman Park.

Oppermann, S. (2016). From material to posthuman ecocriticism: hybridity, stories, nature. In, H. Zapf (ed) handbook of ecocriticism and cultural ecology. Munich: De Gruyter PP 23- 37.

Pike, D. (2014). Comic Complexity in Dr. Seuss's The Lorax: Seuss's Tragic Ecoclassic Morphs into Feature-length Animated Comedy Politicizing Indigenous Knowledge Conservation Practices. Culture and Media: Ecocritical Explorations. Rayson, K. A., Deborah, S. S. & Sachindev, P.S. (eds) (2014). Cambridge: Cambridge Scholars Publishing. PP: 85-105.

Rayson, K.A. (2014). Towards T-Documentary: Critiquing Ecocinema. Culture and Media: Ecocritical Explorations. In, Rayson, K. A., Deborah, S. S. & Sachindev, P.S. (eds) (2014). Cambridge: Cambridge Scholars Publishing. PP: 12-33

Rueckert, W. (1978). Literature and ecology: An experiment in ecocriticism. The Iowa Review, 9(1), 71–86.

Sangili, K. N. (2011, Okt. 13-16). Fasihi Mazingira: Nadharia na Utekelezi katika Fasihi ya Kiswahili. Kongamano la CHAWAKAMA, Hoteli ya Bontana, Nakuru.

Sangili, K. N. & Sabula, M. (2019). Fasihi Mazingira: Mtazamo wa Kinisai katika Riwaya ya Nakuruto. Koja la Taaluma za Insia. Katika, Ponera, A. & Badru, Z. (Wah). Dar es Salaam: Karljamer Pubishers. PP: 338-354.

Sabula, M.A. (2014). Nafasi ya Wanawake katika Uhifadhi wa Mazingira katika Riwaya ya Nakuruto: Mtazamo wa Fasihi ya Ufeministi wa Kiekolojia. (Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngala, O. & Sangili, K.N. (2014). Literary Environmentalism: An Ecocritique of Kiswahili Literature. International Journal of Ecology and Ecosolution Vol 1(2). pp:29-41

Sangili, K.N. (2014). Ubuntuism in the Proverbs of Maragooli Community of Western Kenya. In, Culture and Media: Ecocritical Explorations.In, Rayson, K. A., Deborah, S. S. & Sachindev, P.S. (eds). Cambridge: Cambridge Scholars Publishing pp: 157-167.

Schliephake, C. (2015). Review Essay: Re-mapping Ecocriticism: New Directions in Literary and Urban Ecology. In, Ecozon, vol. 6 (1): 195-207.

Shiva, V. & Mies, M. (1993). Ecofeminism. London: Zed Books.

Singh, J. (2019). Ecocriticism and its' Conceptual Developments: A Sensitive Portrayal through Critics' Pen. International Journal of Research and Analytical Reviews, Vol.6 (1). Pp: 576-579

Ward, S. & Vuuren, K.V. (2014). Exploring Ecocriticism in Australian Film and Television Studies. Culture and Media: Ecocritical Explorations. Rayson, K. A., Deborah, S. S. & Sachindev, P.S. (eds). Cambridge: Cambridge Scholars Publishing pp: 66-84

Warren, K.J. (2000). Ecofeminist Philosophy: A Western Perspective on What It Is and Why It Matters. New York: Rowman and Littelfields Publishers Inc.

Wesonga, E, Ambuyo, B. & Chimerah, R. (2020). Nafasi ya Fasihi katika Kuwasilisha Masuala ya Mazingira Kupitia Riwaya Teule Tikitimaji (2013) na Msimu wa Vipepeo (2006) za K.W. Wamitila. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 2 (2), 54-64.